

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOZA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOZA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC MAKONDA: UKIMPA UJAUZITO MWANAMKE DAR UJIPANGE KWA MATUNZO.

Jopo la Wataalamu kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Maafisa Ustawi wa Jamii, Wanasheria pamoja na Askari Polisi kutoka Dawati la Jinsia wamemuhakikisha Mkoo wa Mkoza wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda kuwa wamejidhatiti vyema kuwasikiliza kinamama waliotelekezwa na hawapatiwi pesa ya matunzo ya mtoto kwenye zoezi la siku tano za kuwapatia msaada wa kisheria kinamama hao linalotaraji kuanza April 09 Mwaka huu.

Akizungumza na wataalamu hao RC Makonda amesema tatizo la wamama waliotelekezwa ni kubwa na limekuwa likisababisha kinamama na watoto kuishi maisha ya tabu na kusababisha ongezeko la watoto wa mitaani na vizazi vya watoto wenye chuki na Baba zao.

RC Makonda amesema lengo la Zoezi hilo sio ugomvi bali ni kumwezesha Mtoto kupata mahitaji ili aweze kuitumia vyema fursa ya elimu bure chini ya serikali ya awamu ya tano.

Aidha RC Makonda amewahimiza wataalamu hao kuhakikisha wanawasikiliza kinamama kwa umakini na kusimamia haki pasipo upendeleo.

Pamoja na hayo RC Makonda amesema wapo kinababa ambao wameanza kutoa fedha ya matunzo ya mtoto baada ya kusikia tangazo ambapo amewasihi kinamama hao kufika April 09 kwa ajili ya kuonana na wataalamu ili waweke makubaliano kwenye mfumo rasmi wa kimaandishi.

**IFIKE HATUA MWANAUME UKIMPA MWANAMKE UJAUZITO BILA
MPANGILIO AOGOPE KAMA ILIVYO KWENYE UBAKAJI.**

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

28/03/2018